

HOTUBA YA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA BWANA GEORGE D. YAMBESI KUMKARIBISHA KATIBU MKUU
KIONGOZI BALOZI OMBENI Y. SEFUE KWENYE UZINDUZI WA WAKALA ZA
SERIKALI TAREHE 11 JULAI, 2012

Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;

Ndugu Makatibu Wakuu na;

Naibu Makatibu Wakuu;

Watendaji Mbalimbali wa Serikali;

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Ushauri za Wizara mliopo;

Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali;

Wakurugenzi;

Ndugu Wanahabari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

Kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kukukaribisha Katibu Mkuu Kiongozi katika hafla hii ya uzinduzi wa Wakala tano za Serikali ambazo ni: Wakala ya Serikali Mtandao; Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao; Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi; Wakala ya Mafunzo ya Mifugo na Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania. Kwa namna ya pekee napenda nikushukuru sana kwa kukubali kwako kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huu wa taasisi hizi muhimu za

Serikali, licha ya majukumu yako makubwa uliyonayo ya Kitaifa. Pili, napenda kuwashukuru wageni wetu wengine wote mliopo hapa kwa kutenga muda wenu ili kuhudhuria hafla hii. Nasema asanteni na karibuni sana.

Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Watendaji wa Wakala na Wageni Waalikwa;

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kama msimamizi mkuu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Sura 245, imeendelea kuziwezesha Wizara mbalimbali katika mchakato wa kubadili baadhi ya majukumu ya Idara na Vitengo vyao kuwa Wakala za Serikali, ili zifanye kazi kwa niaba ya Serikali kwa ufanisi na tija zaidi. Tukio la leo ni ushahidi wa mchakato huo na linatufanya tufikishe jumla ya Wakala thelathini na tano (35) tangu mpango huu ulipoanzishwa mwaka 1999. Wakala hizi zinatakiwa kutumia mbinu za kisasa kiutendaji na za kiuendeshaji ili kuboresha zaidi utendaji kazi na kutoa huduma bora, kwa kiwango na kwa wakati lakini zikiwa kwenye uangalizi wa karibu wa Serikali. Hii inatukumbusha ile dhana maarufu ya '**Eyes On, Hands Off**'.

